

For More Free CSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
MACHI/APRIL 2013
Muda. Saa $2\frac{1}{2}$
Kidato cha 4

MTIHANI WA PAMOJA WA WEZOJE - 2013

(Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari)

Kiswahili

Karatasi ya 3

MAAGIZO

- Jibu maswali manne
- Swalii la Kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki, yaani, Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

SEHEMU A: USAHIRI

Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani

Afya yangu dhahili, mno nataka amani

Nawe umenikabili, nenende sipitalini

Sisi tokea **azali**, twende **zetu** mizumuni

Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani

Tuna dawa za asili, hupati sipitalini

Kwa nguvu za kirijali, Mkuyati uamini

Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani

Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,

Dawa yake ni subili, au zongo huanoni

Zabadili pia **sahali**, kwa maradhi yalo ndani

au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani

Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini

Daktari k'ona mwili, tanena **kensa** tumboni

Visu visitiwe makali, tayari kwa pirisheni

Ukatwe kama fagili, tumbo nyangwe na maini

Nifwateni sipitalini, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi **dhalili**, kutenguliwa tegoni

Yakifika sipitali, huwa hayana kifani

Wambiwa damu kaliti, ndugu msaidieni

Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani

Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, Wakueleze undani.

Maradhiyo ni ajali, yakata vitu thamani

Utete huku wawili, wa manjano na kijani

Matunda pia asali, vitu vyae shamoni

Nifwateni sipatali, na dawa zi langoni?

Maswali

- a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (Alama 2)
- b) Mtanzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili? (Alama 2)
- c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitalini? (Alama 4)
- d) Eleza umbo la shairi hili. (Alama 2)
- e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi? (Alama 2)
- f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi: (Alama 4)
- i) Dhalili
- ii) Azali
- iii) Sahali
- iv) Kensa

SEHEMU B: TAMTHILIA Mstahiki Meya

- 2. Ndugu Meya! Unasahau kuwa wote wafanyakazi wanaogoma ndio wachomwao na jua kutuletea sisi tunaopokea kivulini.
 - a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
 - b) Taja sifa mbili za msemaji (Alama 2)
 - c) Onyesha jinsi wanacheneo wanavyoendeleza juhudzi zao za kupigania haki. (Alama 14)
- 3. Usaliti ni jambo la kawaida katika jamii ya Cheneo. Jadili. (Alama 20)

SEHEMU YA C: RIWAYA: Utengano

- 4. Onyesha jinsi ulaghai unavyoathiri jamii katika riwaya ya Utengano. (Alama 20)
- 5. “Haifai kuiacha fursa hii. Hawa mahaini walitupa nafasi tuwasubu na sisi tulinyamaza kimya...”
 - a) Weka dondo katika muktadha. (Alama 4)

- b) Eleza matukio yaliyojiri baada ya dondoo hili. (Alama 16)

SEHEMU YA D: Damu Nyeusi

6. a) Taja na ueleze sifa tano za Msimulizi wa hadithi ya Mke Wangu. (Alama 10)
b) Jadili migogoro na mayojitokeza katika hadithi ya Mke Wangu. (Alama 10)
7. Jadili madhui yafuatayo jinsi yanavyojitokeza katika hadithi ya Samaki wa Nchi za Joto.
i) Mapenzi na athari zake. (Alama 10)
ii) Matabaka (Alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Taja aina tatu za malumbano ya utani. (Alama 3)
b) Taja na ueleza sifa tatu za malumbano ya utani. (Alama 3)
c) Malumbano ya utani yana umuhimu gani katika jamii. (Alama 4)
d) Eleza sifa zozote tano za mawaidha. (Alama 10)